Mwananchi Newspaper
6th/May/2021

'Tunalomba Mahakama iifute kesi hii kwa kuwa Serikali imeshindwa kuleta mashahidi.'

Wakili, Peter Kibatala

Mashtaka (DPP) ya kuwafungulia mashtaka hayo upya kama ataona inafaa.

Wabunge hao wa viti maalumu ni Halima Mdee, Ester Bulaya na Ester Matiko, aliyekuwa Meya wa Ubungo Jacob Boniface, Patric Assenga, Henry Kilewo na wenzao 21 waliofunguliwa kesi mwaka jana wakikabiliwa na mashtaka saba.

Uamuzi wa kuwafutia kesi umetolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Huruma Shaidi, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kusikiliza ushahidi.

wa na wakili Peter Kibatala na Edson Kilatu walipinga kuahirishwa kwa kesi hiyo na kuiomba mahakama kuifuta kwa kuwa upande wa mashtaka wameshindwa kuleta mashahidi kwa muda mrefu.

Februari 15, 2021 upande wa mashtaka uliwasomea washtakiwa hoja za awali (PH) na kuieleza mahakama wanatarajia kuwa na mashahidi 22.

Hata hivyo, kesi hiyo iliyopangwa kuanza kusikilizwa ushahidi Aprili 5 na Aprili 7, 2021 haikuendelea hadi jana ilipofutwa.

joseph@mwananchi.co.tz

**Rombo.** Jani la sale linalotumika kuomba msamaha kwa mila za Kichaga mkoani Kilimanjaro limeelezwa kuwa chanzo cha kuendeleza matukio ya ubakaji kwa watoto wadogo ambapo kila mwezi zaidi ya watoto 11 hubakwa wilayani Rombo.

Mkuu wa Dawati la Jinsia wilayani humo, Koplo Selestina Malisa akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika kijiji cha Mrere, wa chanzo cha kukwamisha kesi nyingi za ubakaji na kuwa kitovu cha kuendeleza matukio hayo.

Aliyataja maeneo yanayoongoza kwa ukatili wa watoto kuwa ni Tarakea, Mashati, Usseri na Mengwe ambapo watoto wamekuwa

**11**

**Ni matukio ya ubakaji yanayotokea kila mwezi wilayani Rombo mkoani Kilimanjaro.**

matukio hayo hufanywa na ndugu.

"Tunapata shida sana sisi watu wa dawati la jinsia hapa Rombo, unakuta kuna kesi za ubakaji ziko wazi kabisa lakini jamii za watu wa hapa Rombo wamekuwa wakitumia jani la sale na kumalizana mtaani, siku ya siku ikifika unajikuta uko peke yako mahakamani, hakuna mzazi wala mtoto anayeonekana, inaumiza na kutupa wakati mgumu," alisema Koplo Selestina.


**LOSS REPORT.**
**BONDENI FLOWERS LIMITED**

The above-named Company is reporting for the Loss of Certificate of Incentive with number (0224039)01237-01 issued at 15TH day of May 2019 by Tanzania Investment Center.

**Whoever will find this should report to any police station for reference number BNG/RB/115/2021.**


# Patashika Basata, wasanii

Nasra Abdallah, Mwananchi
nabdallah@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Wakati wadau wa muziki na wasanii wakilikosoa Baraza la Sanaa la Taifa (Basata) kwa ukaguzi wa nyimbo za wasanii kabla ya kuachiwa, lenyewe limesema utekelezaji huo ni kwa mujibu wa sheria na lengo ni kutoa madaraja ya nyimbo husika, si kuzifungia.

Akizungumza na *Mwananchi* jana, Kaimu Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Matiko Mniko amesema suala hilo si jipya, bali ni utekelezaji wa sheria namba 23 ya mwaka 1984 ya Baraza la Sanaa la Taifa pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2019.

Alisema kanuni za sheria hiyo zimetoa ufafanuzi kupitia kanuni namba 25 kifungu (1)-(8).

# Serikali kuzipitia sheria kandamizi



"Tunakwenda kuangalia mifumo ya kikodi, kuangalia mifumo ya udhibiti kwa sababu hatutaki kuonekana ni wadhibiti wa sekta ya mawasiliano tu, bali walezi wa sekta hii."

**Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk Faustine Ndugulile.**

Aurea Simtowe, Mwananchi
asimtowe@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Serikali inatarajia kuanza kufanya mapitio ya mifumo yote ya sheria kandamizi katika ukuaji wa sekta ya Mawasiliano na teknolojia ya habari nchini (Tehama).

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk Faustine Ndugulile wakati akizungumza na wanahabari katika mkutano wa Umoja wa Maofisa Watendaji Wakuu wa Kampuni Binafsi nchini (CEOrt) uliofanyika juzi.

Dk Ndugulile alisema nchi inahitaji kampuni zitakazofanya uwekezaji wa utengenezaji wa vifaa mbalimbali vitakavyotumika katika uendelezaji wa Tehama, ikiwemo simu janja na kompyuta mpakato.

Alisema vifaa vingi bado vinaagizwa kutoka nje kama cables na vifaa vingine vya Tehama. "Katika hili tunatarajia kuanza kufanya mapitio ya mifumo yote ya kisheria ambayo inaonekana kuwa kandamizi katika ukuaji wa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari nchini (Tehama).

"Tunakwenda kuangalia mifumo ya kikodi, kuangalia mifumo ya udhibiti kwa sababu hatutaki kuonekana kama wadhibiti wa sekta ya mawasiliano, bali tunataka kuonekana kama tunalea na kukuza sekta hii," alisema Ndugulile.

Alisema hilo pia litafanikiwa kwa kuanza kufanya mabadiliko ya ndani ya wizara kwa sababu wanataka kuiona ikiangazia mahitaji ya Tehama katika miaka ijayo.

Mwenyekiti wa CEOrt, Sanjay Rughani alisema kuanzishwa kwa Wizara ya Teknolojia ni hatua itakayoharakisha ukuaji wa Tehama nchini.

"Intaneti imekuwa ni moja kati ya mahitaji muhimu katika ukuaji wa uchumi wetu. Katika sekta za kibenki tunataka kuongeza uwezo wetu wa kuwafikia watu," alisema.